

MAELEZO MAFUPI YA BAJETI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA KWA MWAKA 2016/2017

1.0 MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YAMWAKA 2016/2017

Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya mwaka 2016/2017 imeandaliwa kukidhi uendeshaji wake na kuiletea maendeleo

a) Mishahara: Jumla ya **Tshs 30,740,945,357.00** zimetengwa ambapo

Tshs 30,704,068,557.00 zinatokana na serikali kuu na **Tshs**

36,876,800.00 zitatokana na makusanyo ya ndani ya Halmashauri

b) Matumizi mengineyo: Jumla ya **Tshs 2,487,539,200.00** zimetengwa

katika kugharamia matumizi mengineyo. Kati ya hizo **Tshs**

1,507,665,000.00 zitatoka serikali kuu na **Tshs 979,874,200.00** zitatokana

na makusanyo ya ndani yatakayokusanywa na Halmashauri. Mambo

yaliyopewa umuhimu katika bajeti hii ni kama ifuatavyo:-

- i. Uendeshaji wa Vikao vya Kamati za kudumu za Halmashauri na vinginevyo ambavyo vinafanyika kwa utaratibu uliopo
- ii. Ununuzi wa mafuta, shajara na ulipaji wa posho za kwenda maeneo ya kazi za miradi na mikutano Vijijini na mkoani na kwingineko kama inavyotarajiwa kutokea
- iii. Ununuzi wa vitendea kazi kama vile gari dogo (1) kwa shughuli za Maliasili.

c) Miradi ya Maendeleo: Jumla ya **Tshs 4,277,044,000.00** zimetengwa

kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya hizi **Tshs**

2,713,885,000.00 zitatoka serikali kuu na wadau wengine wa maendeleo

na **Tshs 1,563,159,000.00** zitatokana na makusanyo ya mapato ya ndani.

Bajeti ya maendeleo imezingatia kuwa;

- i. Miradi ya sekta za matokeo makubwa sasa imepewa kipaumbele ili kuharakisha maendeleo ya wananchi
- ii. Miradi ambayo ilikuwa inaendelea imepangwa ili ikamilike na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi wa maeneo inakotekelezwa.
- iii. Miradi iliyopendekezwa na wananchi na wananchi walishaanza kutekeleza imepewa kipaumbele katika bajeti hii
- iv. Miradi inayotarajiwa kuongeza uzalishaji imepewa kipaumbele ili kuongeza pato la wananchi na wilaya kwa ujumla
- v. Kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizo ya UKIMWI imepewa kipaumbele ili kuendeleza mapambano yaliyokwisha anza

3.0 Halmashauri imepanga bajeti kwa muhtasari ufuatao

NA	ENEO	MAPATO YA NDANI	SERIKALI KUU	JUMLA
1	MISHAHARA	36,876,800.00	30,704,068,556.00	30,740,945,357.00
2	MATUMIZI YA KAWAIDA	979,874,200.00	1,507,665,000.00	2,487,539,200.00
3	MIRADI YA MAENDELEO	1,563,159,000.00	2,713,885,000.00	4,277,044,000.00
JUMLA		2,579,910,000.00	34,925,618,556.00	37,505,528,557.00

Sophia J. Kumbuli
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya
CHUNYA